

SAUTI YA WATU

Tanzania Daima

BSSN 0858 9762 TOLEO NA. 3150 IJUMAA, JULAI 19, 2013 TSH. 500 KSH. 50

RAMADHANI 10



'Hatuna haja na meya wa Arusha'

Na Grace Macha, Arusha

SUALA la nafasi ya meya wa jiji la Arusha limechukua sura mpya, baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kudai kuwa sio ajenda yao ya sasa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu wa Kanda ya Kaskazini wa Chadema, Amani Golugwa, alipozungunza na waandishi wa habari jana jijini hapa kwamba kwa sasa madiwani wa chama hicho wamejipanga kurweka mikakati ▼3

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akiwashirikisha wananchi wa mji wa Songea na vitongoji vyake, kama wanakubaliana na mazmazi ya Kamati Kuu ya chama hicho ya kutimarisha ulinzi kwa viongozi wake kwa kuwapatia mafunzo vijana, wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Songea juzi. (Na Mjiwa Picha Wetu)

Sasa vita mpya Chadema, CCM

- Picha za marehemu zaliza wengi
- Tendwa aonywa, aambiwa ole wako

Na Waandishi Wetu

VYAMA vikubwa viwili hasimu hapa nchini, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) vimeingia

katika 'vita' mpya.

Wakati CCM ikituhumiwa kutumia dola na msajili wa vyama vya siasa 'kukishikisha' adabu Chadema, likiwamo tamko zito la kutaka kukifuta kwa madai ya ▼4



Nyerere: JK ataje wauza 'unga'

Na Mwandishi Wetu

KUCHAFUKA kwa Tanzania kimataifa ikituhumiwa kuwa 'lango' la kusafirisha dawa za kulevya kumewalazimisha wanasiasa kumtaka Rais Jakaya Kikwete kuyakamata haraka vigogo wanaohusika na biashara hiyo.

"Ukinywa wa rais unaweza kuchukuliwa kuwa serikali yake haina tena ubavu wa kupambana na wauza unga, jambo ambalo ni hatari kwa vijana wetu."

Mmoja wa wanasiasa hao, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, Vincent Nyerere (Chadema), amelazimika jana kutoa taarifa kwa vyombo vya habari

nchini akimwomba Rais Kikwete kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika ambao aliwahi kudai anawajua kwa majina.

Nyerere ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani, katika taarifa yake alisema Rais Kikwete ndiye aliyeutangazia umma kuwajua wahusika ya biashara hiyo, lakini ameshindwa kuwataja, badala yake kumekuwa na ▼4

